# MAPITIO YA MWENENDO WA SOKO KWA WIKI
# 14 FEBRUARI 2025

**KARIBUNI TENA KATIKA KIPINDI CHETU CHA KILA WIKI KINACHOKUHABARISHA KUHUSU MWENENDO WA SOKO LA HISA LA DAR-ES-SALAAM, NA KULETWA KWENU NA VERTEX INTERNATIONAL SECURITIES, PAMOJA NANYI LEO NI MIMI, FRANCO ATILYO**

Kwa wiki inayoishia tarehe 14 Februari 2025, mauzo katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) yaliongezeka kwa asilimia 24.72 kutoka TZS 6.9 bilioni hadi TZS 8.67 bilioni. Kiasi cha hisa zilizouzwa kilionezeka pia kutoka hisa milioni 5.3 hadi hisa milioni 14.27 sawa na asilimia 363.72.

Jumla ya Mtaji wa Soko ulipungua kwa asilimia 0.34 kutoka TZS 18.97 trilioni hadi trilioni 18.90. Mtaji wa Soko la Ndani nao ulipungua kwa asilimia 0.02, hadi TZS 12.602 trilioni kutoka TZS 12.604 trilioni kutokana na kupungua kwa bei ya hisa za DCB, DSE, NICO na NMB.

Vodacom imeongoza kwa mauzo ya hisa wiki hii ikirekodi TZS 4 bilioni, ambayo ni 46.25% ya mauzo yote ikifuatiwa na CRDB kwa asilimia 37.88 ya mauzo yote.

Kuhusu bei, hisa za CRDB ziliongezeka kwa TZS 10 wakati za DCB zilipungua kwa TZS 5 huku za DSE nazo zilipungua kwa TZS 20 na za MBP zikiongezeka kwa TZS 10. Hisa za NMB zilipungua kwa TZS 100 huku za NICO zikipungua kwa TZS 40 na zile za TPCC zilipungua kwa TZS 140.

Vodacom iliongoza kwa idadi ya kubwa ya hisa zilizouzwa kwa asilimia 62.37 sawa na hisa milioni 8.9 ikifuatiwa na CRDB kwa asilimia 32.45. Jumla ya hisa milioni 9.34 za CRDB, TCC Vodacom na NMB ziliuzwa kupitia kaunta ya makubaliano ya kabla huku wawekezaji wa nje wakiongezeka kiasi wiki hii. Tunatarajia kuongezeka kwa mwitikio utakaoakisi kwenye mauzo ya hisa na bei kwa wiki zijazo.

Katika wiki kulikuwa na miamala 80 kwenye soko la hatifungani, ambapo soko lilisajili takribani TZS 53.39 bilioni.

Mnada wa dhamana za serikali za muda mfupi uliofanywa na Benki Kuu ya Tanzania tarehe 12 Februari 2025, ulisajili zabuni 104 ambapo zabuni 84 zilifanikiwa na kukusanya kiasi cha TZS 21.79 bilioni.

**MPAKA HAPO TUMEFIKIA MWISHO WA MAPITIO YA SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM KWA WIKI ILIYOISHIA IJUMAA YA FEBRUARI 14, 2025. MPAKA WAKATI MWINGINE MIMI NI FRANCO ATILYO**